WiLDAF

Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)

# ATHARI ZA KIUCHUMI ZA UKATILI MAJUMBANI

## Haja ya Kuwa na Sheria Dhidi ya Ukatili Majumbani

### Muhtasari wa Sera

**Suala la: 3**

Septemba, 2021

Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)

# ATHARI ZA KIUCHUMI ZA UKATILI MAJUMBANI

## Haja ya Kuwa na Sheria Dhidi ya Ukatili Majumbani

### Muhtasari wa Sera

**Suala la: 3**

**Septemba, 2021**

## UTANGULIZI

Ukatili majumbani ni ukatili unaofanywa mara nyingi na mtu katika mazingira ya nyumbani dhidi ya mtu mwingine anayeishi katika mazingira hayo ya nyumba moja. Ukatili majumbani unaweza kuwa wa kimwili, kihisia, kingono, kisaikolojia au kiuchumi.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Umoja wa Mataifa inayoitwa "Athari za Kiuchumi za Ukatili Dhidi ya Wanawake imebaini kwamba duniani kote, ikiwemo Tanzania waathirika wakubwa wa vitendo vya ukatili majumbani ni wanawake na watoto. Kwa mujibu wa ripoti hiyo athari za ukatili majumbani ni pamoja na gharama za moja kwa moja kwa muhanga kama vile huduma za matibabu ya majeraha, gharama za kulipa mwanasheria pamoja na mali iliyopotea au kunyang'anywa kutokana na ukatili. Vile vile ripoti hiyo imeonyesha kwamba athari za ukatili dhidi ya wanawake haziishi tu kwa mtu binafsi bali huathiri uchumi wa nchi kama kuongeza bajeti ya kushughulikia wahanga wa ukatili, kupoteza mapato kwa sababu ya wanawake kushidwa kufanya kazi au biashara pamoja na kulipa watoa huduma wa ukatili wa kijinsia.

Idadi kubwa ya wahanga wa ukatili wa majumbani hawatoi taarifa ya matukio hayo kwa mamlaka husika kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo tamaduni za kijamii ambazo zinamtaka mwanamke kuwa mvumilivu. Lakini pia shinikizo kutoka kwenye familia zao ambapo mara nyingi wanawake huambiwa mambo hayo yamalizwe nyumbani. Vile vile Wahanga wengine hawaripoti matukio ya ukatili majumbani kwa sababu ya hofu ya kulipiziwa kisasi kutoka kwa waume zao, hofu ya kupoteza msaada wa kifedha kutoka kwa wenza wao, lakini pia hofu ya kunyang'anywa Watoto.

Ingawa Serikali ya Tanzania imetunga sheria na miongozo mbalimbali ya kukabiliana na ukatili dhidi ya wanawake, lakini sheria hizo bado zinamapungufu hasa katika kuwaadhibu wahalifu wa ukatili huo.
Muhtasari huu wa sera umeandaliwa kutokana na mapitio ya tafiti mbali mbali zinazoonyesha hali ya kiuchumi ya wanawake na wasichana ambayo inaweza kusababishwa na ukatili majumbani nchini Tanzania. Pia muhtasari huu unatoa mapendekezo kwa watunga sera kuona haja ya kutunga sheria dhidi ya ukatili majumbani ili kusaidia kupunguza ukubwa wa tatizo.

## HALI YA KIUCHUMI KWA WANAWAKE NA WASICHANA

Jukwaa la Uchumi Duniani lilibaini kwamba kuna uhusiano kati ya ukatili majumbani na hali ya kiuchumi kwa wanawake na wasichana. Jukwaa hilo pia linatabiri kwamba pengo la kijinsia halitamalizika kabisa hadi mwaka 2186 kama nchi hazitaweka mikakati ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia. Nchini Tanzania,wanawake wanakabiliwa na changamoto nyingi kwenye kujikwamua kiuchumi zikiwemo upatikanaji wa rasilimali ardhi, ushiriki mdogo wa wanawake katika ngazi zote za kufanya maamuzi, ukatili wa kijinsia, wanawake kukosa elimu na ujuzi sahihi, pamoja na wanawake kuwa katika nafasi za chini kwenye kazi zenye kipato. Kwa mujibu wa Ripoti ya Nchi juu Usawa wa Kijinsia ya 2019, Tanzania ilishika nafasi ya 125 kati ya nchi 155 ikiwa na kiwango cha 0.547. Aidha, changamoto za kushindwa kufikia malengo ya usawa wa kijinsia zinachochewa na ukatili majumbani ambao unaminya haki za kiuchumi kwa wanawake katika ngazi ya familia na jamii.

Utafiti wa shule za wasichana katika mikoa ya Dodoma, Singida, Lindi na Pwani ulionyesha kuwa kazi nyingi za nyumbani ni moja ya sababu inayosababisha wasichana wengi kukatisha masomo. Utafiti huo ulibaini kwamba, asilimia 76 na asilimia 63 ya wasichana kutoka Singida na Pwani wanakabiliwa na ukatili majumbani ikiwemo kazi nyingi bila usaidizi. Majukumu ya ndani yaliyoripotiwa ni pamoja na kuchota maji, kukusanya kuni, kuwatunza watoto, kuchunga mifugo, shughuli za kilimo, kuangalia biashara ya mzazi nk. Wanawake wengi kukosa elimu stahiki inachangia kuongeza umasikini pamoja na utegemezi kutoka kwa wanaume.

Ukatili dhidi ya wanawake na wasichana pia hupunguza kasi ya taifa katika kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya dunia kwa kuathiri afya ya wanawake na wasichana, elimu, na kupunguza ushiriki wao katika kazi za uzalishaji. Aidha, inakiuka haki za binadamu za wanawake na wasichana na inaweza kuharibu ustawi wa kiuchumi kwa muda mrefu.

Wanawake wa Tanzania wanamchango mkubwa katika uchumi wa nchi hivyo ni muhimu kuwa na sheria itakayolinda wanawake dhidi ya ukatili majumbani.

## ATHARI ZA KIUCHUMI ZA UKATILI MAJUMBANI

Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS), 2015-2016 umebaini kuwa;

- Asilimia 40 ya wanawake wote walio olewa wamewahi kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kimwili, kingono, au kihisia kutoka kwa wenzi wao. Ukatili majumbani hauathiri tu asilimia 40% ya wanawake na wasichana, bali pia huathiri maendeleo ya kiuchumi ya nchi. Tafiti mbali mbali zinaonesha kwamba ukatili majumbani unaathari kubwa kwenye uchumi wa wanawake kama ilivyoelezwa hapo chini;

### a) Nguvu kazi na kipato kwa wanawake.

Wanawake na wasichana ambao mara kwa mara wanapitia vitendo vya ukatili wa majumbani huathiriwa katika aina ya kazi ambayo wanaweza kufanya, na pia kufanya kazi zenye kipato cha chini au zisizo na kipato kabisa. Kwa mujibu wa Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS) 2015/2016 ulibaini kuwa

- Zaidi ya wanawake 6 kati ya 10 walioolewa wenye umri kati ya miaka 15-19 na karibu nusu ya wanawake walioolewa kati ya umri wa miaka 20-24 hawalipwi kwa kazi wanazofanya.
  - ✓ Kati ya wanawake walioko kwenye ndoa na wanaofanya kazi ni asilimia 9 tu ya wanawake wanaopata malipo Zaidi ya waume zao kwa kazi ambazo wanafanya. Mwaka 2020, kupitia ufwatiliaji wa haki za binadamu na vyombo vya habari, mauaji 32 ya wanawake yalirekodiwa nchini Tanzania, ambapo 23 yalichochewa na wivu wa mapenzi. Mauaji dhidi ya wanawake hupunguza nguvu kazi ya uzalishaji kiuchumi na huathiri uchumi wa Taifa.

Hivyo, ili kuongeza nguvu kazi ya taifa, Pamoja na kukuza kipato cha wanawake ipo haja ya kukomesha Ukatili majumbani.

### a) Wanawake na umiliki wa rasilimali

Mara nyingi katika jamii zetu mwanamke wana nafasi ndogo ya umiliki wa rasilimali kama vile ardhi, mifugo, au mazao ya biashara kwa sababu ya ukatili wa kiuchumi. Licha ya mabadiliko kadhaa ya sheria za Ardhi, umiliki wa ardhi kwa wanawake nchini Tanzania unaendelea kuwabagua wanawake kwa sababu ya desturi na sheria za kimila. Haki za ardhi kwa wanawake zimepuuzwa, na ili mwanamke aweze kumiliki na kutumia ardhi itategemea uhusiano wake na mumewe. Kwa Mujibu wa Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS) 2015/2016:

- Asilimia 9 tu ya wanawake waliripoti kumiliki nyumba peke yao, huku asilimia 38 ya wanawake waliripoti kumiliki pamoja na wenzi wao.

- Vile vile, asilimia 34 ya wanawake waliripoti kwamba wanamiliki ardhi peke yao au pamoja na wenzi wao.
- Wanawake kukosa umiliki wa makazi/nyumba/ardhi huongeza tabaka kubwa la wanawake tegemezi na wengi wao hawatoi taarifa za ukatili wa kijinsia kwenye vyombo vya sheria kwa kuhofia kufukuzwa katika nyumba au ardhi wanayoitumia kwa uzalishaji wao.

Kutokomeza ukatili majumbani itakuwa na manufaa kwa kuongeza upatikanaji wa rasilimali kwa wanawake na hivyo kuongeza uzalishaji na uhuru wa kifedha baina ya wanawake na wasichana.

### b) Wanawake na Upatikanaji wa Mitaji

Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) 2016/17-2021/22, katika eneo la kwanza la utekelezaji unalenga kuhakikisha uchumi wa kaya unaimarika kwa kuwapa wanawake fursa ya kupata mikopo ya kifedha kwa kupitia mifuko ya halimashauri. Aidha, mpango huo unajaribu kuondoa vikwazo ambavyo kwa muda mrefu vimewazuia wanawake kupata mitaji yenye riba nafuu, ukizingatia wanawake hawana ardhi au rasilimali nyingine za kuweka dhamana kwenye mabenki.

Licha ya jitihada hizo za serikali, idadi ya wanawake wanao nufaika na mikopo hiyo bado ni wachache kwa sababu ya ukatili majumbani. Mara nyingi wanawake hawana maamuzi juu ya kujihusisha na aina yoyote ya kiuchumi katika ngazi ya familia. Lakini pia idadi ya wanawake wanaopata mikopo kupitia taasisi nyingine kama vile Benki na Taasisi nyingine za fedha ni ndogo. Vile vile wanawake katika sekta ya uzalishaji wanakabiliwa na vikwazo vingine kama udhibiti wa kiuchumi ndani ya familia kutoka kwa waume zao. Mara nyingi wanaume huamua biashara gani ya kufanya na jinsi gani wanapaswa kupata mitaji ya kifedha kwa ajili ya biashara. Wakati mwingine, wanawake wananyimwa kujihusisha na vikundi vya kiuchumi kama VICOBA na Vikundi vingine vya hisa.

Kukosekana kwa sheria inayokataza vitendo vya udhibiti wa kiuchumi baina ya wenza husababisha tatizo hili kuendelea kuwa kubwa na kuminya haki za wanawake kujihusisha na maswala ya kiuchumi au umiliki wa mali binafsi.

## c) Elimu na ujuzi duni kwa Wanawake

Azimio la Beijing na Jukwaa la kuchukua hatua linasisitiza kuwa elimu ni moja ya njia muhimu sana katika uwezeshaji wa wanawake barani Afrika. Wanawake wengi nchini hasa vijijini hawana elimu kwa sababu ya ukatili majumbani. Tanzania imeweka mikakati ya kuhakikisha kwamba wanawake wanapata elimu sawa na wanaume kwa kutekeleza sera za elimu bure kuanzia mwaka 2015. Pia kufanyia maboresho Sheria ya Elimu kukataza ndoa na mimba kwa wasichana wa shule. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 bado inaruhusu wasichana kuolewa wakiwa na umri wa miaka 14 kwa ruhusa za mahakama na 15 kwa idhini ya wazazi. Nchi nyingine, kama vile Kenya, Malawi nk zinahusisha ndoa za utotoni kama aina mojawapo ya ukatili majumbani ambayo ina athari za kiafya, kijamii na kiuchumi kwa maisha ya wanawake na wasichana. Ndoa za utotoni zina matokeo ya kiuchumi kwa wasichana na wanawake kama ifuatavyo;

- ***Uzazi na ukuaji wa idadi ya watu***: Wasichana wanaoolewa mapema wana hatari ya kupata watoto mapema kuliko wenzao ambao wamechelewa kuolewa. Vile vile wanauwezekano wa kupata Watoto wengi zaidi. Kuwa na watoto wengi kunaweza kuchangia ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya watoto na familia kwa ujumla. Kwa mujibu wa utafiti iliyofanywa na kitengo cha kimataifa cha utafiti wa wanawake (2018), Pamoja na Benki ya Dunia, ulibaini kwamba kutokomeza ndoa za utotoni kunaweza kupunguza uzazi kwa asilimia kumi na moja (11%), na kupunguza ukuaji wa idadi ya watu. Pia, kupungua kwa idadi ya watu katika familia kunaweza kuongeza upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya mahitaji ya nyumbani kama vile chakula, mavazi, malazi, elimu, huduma za afya, na gharama nyingine.

- ***Ukosefu wa elimu na ujuzi kwa wasichana na wanawake:*** Takwimu za Tanzania zinaonyesha kuwa, mwanamke mmoja kati ya wanawake ishirini wenye umri kati ya miaka 15-49 walioolewa wakiwa na umri mdogo wamesoma hadi kidato cha nne ikilinganishwa na asilimia 28 ya wale walioolewa na miaka 20 au zaidi. Vivyo hivyo, kuolewa katika umri mdogo kunasababisha kuwa na tabaka la wanawake na wasichana wenye elimu na ujuzi duni. Kwa Mujibu wa ripoti ya Benki ya Dunia (2018), Ilibaini kwamba ndoa za utotoni hupunguza uwezekano wa wasichana kumaliza shule ya sekondari kwa asilimia 4 hadi sita. Pia ilibainisha kuwa wasichana kukosa elimu kunaongeza uwezekano wa kuwa na kipato cha chini kipindi cha utu uzima wao. Vile vile ndoa za utotoni na ukosefu wa elimu husababishia taifa hasara ya asilimia moja ya mapato kwa kupunguza nguvu kazi ya taifa

- ***Kupunguza nguvu kazi:*** Kama ilivyoelezwa hapo juu, wasichana waliolewa mapema wana uwezekano wa kuwa na watoto wengi zaidi, hivyo usumbufu wa kujifungua mara kwa mara pamoja na ulezi unaweza kuathiri aina za kazi ambazo wanawake wanaweza kufanya. Mara nyingi majukumu yakulea huwafanya wanawake kubaki katika nafasi za chini kwenye ajira au nafasi zisizo na malipo. Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa kitengo cha kimataifa cha utafiti wa wanawake (2018), Ndoa za utotoni, kwa wastani zinapunguza kipato cha wasichana kwenye utu uzima wao kwa asilimia tisa (9%).

- Kutokomeza ndoa za utotoni kunaweza kuongeza nguvu kazi,uzalishaji na kipato kwa wanawake (ICRW 2018).

### d) Gharama za Huduma za Kiafya zitokanazo na Ukatili Majumbani

Ripoti ya Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya (TDHS), 2015-2016 umebaini kuwa;

- Asilimia70% ya wanawake ambao wamewahi kupata ukatili wa kimwili au kingono wamepata aina moja au zaidi ya majeraha kama kukatwa, kupata michubuko, au maumivu makali sehemu za mwili.
- Vile vile, asilimia 15 ya wanawake hao walipata majeraha makubwa, kama mifupa kuvunjika, kuvunjika meno, au majeraha mengine makubwa kutokana na ukatili kutoka kwa wenza wao. Majeraha yanayosababishwa na vitendo vya ukatili yanagharimu huduma za afya kwa kutoa matibabu kwa wahanga.
- Mpango Mkakati wa Taifa wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA), unakadiria kuwa gharama za kukabiliana na ukatili nchini Tanzania kuanzia mwaka 2016/17 - 2021/22 ni jumla ya bilioni **27,391,620,000** kwa ajili ya huduma za moja kwa moja za matibabu na huduma za kisaikolojia. Pia gharama hizo zitahusishakuandaa mwongozo wa kushughulikia maswala ya ukatili, mafunzo ya watoa huduma kama vile Maafisa Ustawi wa Jamii, Polisi kitengo cha dawati la jinsia, kuimarisha taratibu za rufaa, kuanzisha vituo vya mkono kwa mkono, Madawati ya Polisi ya Jinsia na watoto Pamoja na nyumba salama.
- Mbali na gharama kwa Serikali, ukatili majumbani una gharama nyingine kwa wanawake ambapo hutumia fedha nyingi kutibu majeraha yanayosababishwa na ukatili majumbani.

### e) Ongezeko la Kiwango cha Utegemezi wa kiuchumi kwa Wanawake na Wasichana

Tanzania ni nchi ya kipato cha uchumi wa kati, ambapo idadi ya wanawake ni milioni 54.2 sawa na asilimia 51.9% na wanaume milioni 27.7 sawa na asilimia 48.9%. Kwa mujibu wa ripoti ya Umoja wa Mataifa Kitengo cha Wanawake, (UN-Women), umaskini ni changamoto kubwa nchini Tanzania, ambapo zaidi ya nusu ya idadi ya wanawake (60%) wanaishi katika umaskini uliokithiri. Umaskini miongoni mwa wanawake unaweza kusababishwa na ukosefu wa maamuzi ya kiuchumi kwa wanawake. Ongezeko kubwa la wanawake maskini nchini inaweza pia kuwa matokeo ya kukosa maamuzi hasa katika faida ya uzalishaji ambapo nguvu kazi yao imetumika. Kwa mfano baadhi ya maeneo nchini Tanzania maamuzi juu ya uuzaji wa mazao hufanywa na wanaume, huku wanawake wakiachwa kama wazalishaji tu.

Wanawake wanaopitia ukatili majumbani wanauwezekano mkubwa wa kushindwa kujiamini, kufanya kazi za uzalishaji na kazi za kujipatia kipato. Hali hii inazidi kuongeza idadi ya wanawake na wasichana tegemezi katika jamii.

## UMUHIMU WA SHERIA YA UKATILI MAJUMBANI NCHINI TANZANIA?

- Kama ilivyoelezwa hapo awali Serikali ya Tanzania imeadhimiria kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini Tanzania kupitia MTAKUWWA. Licha ya dhamira hiyo, Tanzania bado haina sheria dhidi ya ukatili majumbani. Kukosekana kwa sheria hiyo kunafanya tatizo kuendelea kuwa kubwa nchini Tanzania. Matumizi ya sheria za kimila yanaendelea kuwabagua wanawake nchini na kuendeleza vitendo vya ukatili majumbani.
- Sheria kama hizi hukandamiza wanawake katika kumiliki rasilimali na kuzitumia katika kujikwamua kiuchumi, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 bado inamapungufu kwa kushindwa kutoa adhabu kwa wahalifu, lakini pia kueleza aina nyingine za ukatili kama vile ukatili wa kiuchumi, kisaikolojia na kingono. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa na sheria nyingine kama Sheria maalumu ya Makosa ya Kujamiiana, 1998, bado hazielezi ukatili majumbani kama ni kosa kisheria na kuendelea kuacha mwanya kwa ukatili huu kutokea.

## MAPENDEKEZO

1. Serikali ichukue hatua kutunga sheria dhidi ya ukatili majumbani. Sheria hiyo inapaswa kukemea ukatili wa nyumbani kuwa ni kinyume cha sheria na kutoa adhabu dhidi ya wahalifu
2. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine, inapaswa kutenga bajeti ya kuongeza idadi ya nyumba salama kwa wanawake na watoto wanaokabiliwa na ukatili majumbani, kwa lengo la kuboresha ulinzi kwa wahanga.
3. Watoa huduma za afya na kijamii wanapaswa kuimarisha mifumo yao ya utoaji wa huduma ili kuimarisha upatikanaji wa takwimu za Ukatili majumbani, bila kujali kama ukatili huo uliripotiwa kwenye mamlaka nyingine au la.
4. Utafiti wa kitaifa ufanyike ili kuchunguza athari zaidi za ukatili majumbani katika uchumi wa mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Pia, utafiti huo uonyeshe uchambuzi wa gharama za huduma za afya kwa taifa na mtu binafsi.
5. Ushirikiano kati ya watoa huduma kwa wahanga wa ukatili uboreshwe ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za matibabu na huduma nyingine kwa wahanga wa ukatili kwa haraka zaidi.
6. Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine inapaswa kuanzisha/kutekeleza mpango maalumu wa uwezeshaji wa kiuchumi kwa wanawake na wasichana ili kuhakikisha wanawake wanapata rasilimali na mikopo.

### Kuhusu Shirika la Wanawake Katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF)

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika, ni mtandao wa mashirika ya watu binafsi katika Bara la Afrika ambao unafanya kazi za kupinga haki za wanawake, kujitolea kukuza na kuimarisha mikakati inayounganisha sheria na maendeleo ili kuongeza ushriki wa ushawishi wa wanawake katika mikakati na pia kueneza chachu hiyo katika ngazi ya jamii, kitaifa na kimataifa.

WiLDAF ilisajiliwa nchini Tanzania mnamo mwaka 1997 chini ya Sheria ya Makampuni Sura ya 212 kama Shirika lisilo la kiserikali, lisilo la kisiasa na lisilojiendesha kwa faida.

WiLDAF Tanzania ina njozi ya kuona jamii ya Tanzania inayoheshimu haki za binadamu za wanawake. Misheni ni kujenga ni kujenga mtandao imara kwa

ajili ya kukuza heshima kwa haki za binadamu za wanawake kupitia utetezi, usambazaji na uangalizi wa vyombo mbalimbali vya kitaifa na kimataifa pamoja na mpango wa dharura wa kuitikia ukatili wa kijinsia katika ngazi zote wakati huo huo ikihusisha sheria na maendeleo.

## Kuhusu Mradi wa Uchechemuzi kwa Kutumia Takwimu (DDA)

Mradi wa uchechemuzi kwa kutumia Takwimu (DDA) ni mradi unaofadhiliwa na Shirika la Kimataifa liitwalo Freedom House pamoja na PACT Tanzania.

Mradi huu ambao ni wa miaka mitano unakusudia pamoja na mambo mengine kutumia takwimu kama sehemu ya kushawishi mabadiliko ya Sera na Sheria ambazo zinalinda na kutetea haki za binadamu.

Mradi huu unafanya kazi kwa kupitia vikosi kazi (WGs) mbalimbali. WiLDAF inaratibu kikosi kazi namba mbili (WG2) ambacho kimejikita katika kusimamia haki za Wanawake,Watoto, Vijana na watu wenye ulemavu.

## SHUKRANI

Taarifa hii fupi ni mchango wa watu binafsi, mashirika na wanachama wa kikosi kazi namba 2 ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa taarifa hii.

Kwa niaba ya kikosi kazi namba 2 (WG2), WiLDAF inapenda kutambua juhudi iliyofanywa na muandishi Bwana Idd Rajabu Mziray kwa kujitolea kwake katika kuandaa rasimu ya awaliya taarifa hii fupi.

Vile vile tunatoa shukrani kwa Mkurugenzi wa WiLDAF Anna Kulaya kwa kuhariri taarifa hii fupi.

WiLDAF inapenda kuwashukuru wafuatao kwa kupitia na kuchangia katika kuboresha taarifa hii fupi; Bi Zakia Msangi, Bi Miriam Azaria, Asajile Mwakyusa, Simoni Songeraeli, Michael Lwakatare pamoja na Bi. Anneth Mushi.

Mwisho, shukrani ziende kwa wanachama wa WG2 ambao wameshiriki kikamilifu katika kuandaa taarifa hii fupi kama ifuatavyo;

1. Women in Law and Development in Africa (WiLDAF),
2. Tanzania Child Right Forum (TCRF),
3. Tanzania Domestic Workers Coalition (TDWC),
4. Mwanza Children and Youth Network (MCYN),
5. Tanzania Early Childhood Development Network (TECDEN),
6. Zanzibar Female Lawyers Association (ZAFELA),
7. Tanzania Association for children Advancement (ZACA),
8. Women Legal Aid Centre (WLAC),
9. Women with Disability Network (SHIVYAWATA),
10. Youth Partnership countrywide (YPC),
11. Gender and Adolescence Initiative (GAI)
12. Vijana Pambana Pata Maendeleo Rukwa (VIPAMARU),
13. Jitambue Lembuka,
14. Health Integrated Multispectral Services (HIMS),
15. Women Development for Science and Technology Association (WODSTA).

## MAREJEO


1. Ripoti ya Utafiti wa Shule za Wasichana katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Lindi na Pwani Mradi wa Haki za Wasichana 2017.
2. ICRC, 2018: "Athari za kiuchumi za ndoa za utotoni: matokeo muhimu julai 2018).
3. Myamba, Flora Peter, 'Harakati za Haki za Ukatili majumbani Tanzania: Uchunguzi' (2009). Dissertations.
4. Human Development Trust (HDT). Mwezi wa Juni 2011. Mapungufu katika Sera na Sheria zinazoendeleza ukatili wa kijinsia nchini Tanzania. [Imepitiwa 2 Julai 2021].
5. USAID (2008), Ukatili wa kijinsia nchini Tanzania: Tathmini ya sera, huduma, na hatua za huduma-2008.
6. Tanzania: Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya, (TDHS) 2015/2016.
7. Shirikisho la Wanawake Wanasheria Tanzania, Septemba 2014: Mapitio ya Sheria na Sera zinazohusiana na Ukatili wa Kijinsia Tanzania Bara.
8. Kitrina Miller (2021), Kuathiri Ustawi wa Uchumi wa Wanawake: Ukatili dhidi ya wapenzi wa Karibu- 2021.
9. WAO, 2019, Ukatili majumbani na Shirika la Misaada ya Wanawake wa Umaskini (WAO) | Desemba 2019.
10. Serikali ya Tanzania: Mpango Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA), 2016/17-2021/22.
11. https://africa.unwomen.org/en/where-we-are/eastern-and-southern-africa/tanzania.

ISBN 978-9912-9860-2-2
9 789912 986022

**Imechapishwa na WiLDAF, 2021**

Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo barani Afrika
Eneo la Mikocheni A. Mtaa wa WiLDAF, Block F. Ploti Na. 635.
S.L.P 76215, Dar es salaam, Tanzania

**Simu:** +255222701995,
**Barua pepe:** wildaftanzania@gmail.com / info@wildaftanzania.or.tz
**Tovuti:** www.wildaftanzania.or